COMPETENCE BASED ASSESSMENT
MONITORING LEARNERS PROGRESS

5

JINA: _____.

SHULE: _____.

NAMBA YA MTIHANI: _____TAREHE: _____.

KISWAHILI

Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali yatuatayo

(Mwalimu na mwanafunzi wanajadiliana kuhusu umuhimu wa kuyatunza mazingira)

Mwalimu: Hamjambo wanafunzi?

Wanafunzi : (Wakiamka sawia) Hatujambo mwalimu, shikamoo.

Mwalimu : Marahaba (anawaashiria wakae. Wote wanaketi na kushukuru) Naam, leo ningependa tuzungumze kuhusu namna na umuhimu wa kuyatunza mazingira kwa hivyo....

Matayo : (Anaunyanyua mkono wake) samahani mwalimu mazingira ni nini?

Mwalimu : (Akitabasamu) Matayo huishi vituko! Ndilo nililotaka kueleza. Mazingira ni yale yote yanayotuzunguka. Hebu pendekezeni njia mbalimbaliza kuyatunza mazingira.

Manyanga : Nadhani ni vyema kukata nyasi ndefu ilikuharibu makao ya mbu.

Kaisari : Ni vyema pia kutunza vyanzo vya maji kama vile mito, chemichemi mabwawa na maziwa.

Pendo : Nikiongezea, si vyema kutumia mbolea nyingi zaidi hasa za madukani ili tusiyaathiri maji na udongo.


Mwalimu : Nimefurahia michango yenu. Zipo njia nyingi za kuyatunza mazingira. Kimsingi, umuhimu wa kuyatunza mazingira ni kuwafanya viumbe waishi maisha salama.

1. Mazungumzo haya yaliandaliwa majira ya saa ngapi?

   A. Saa sita aduhuri
   B. Saa mbili asubuhi
   C. Saa kumi jioni
   D. Hatujaelezwa

2. Ili kuonyesha heshima kuu, walimu alipowaamkia wanafunzi wote?
   A. Walisimama ili kupokea salamu yake
   B. Walitaka kujua maana ya majadiliano
   C. Walitaka kujua maana ya mazingira
   D. Walitaja umuhimu wa kuishi katika mazingira safi
3. Ni mwanafunzi yupi aliyemkatiza mwalimu alipokua akiongea
   A. Manyanga
   B. Matayo
   C. Kaisari
   D. Pendo
4. Kulingana na mazungumzo haya, yote yanayotuzunguka ndiyo?
   A. mzingira
   B. miti
   C. hewa
   D. mazingara
5. Mwishoni, mwalimu alifurahishwa na nini?
   A. Heshima ya wanafunzi
   B. Umuhimu ya kuyatunza mazingira
   C. Michango ya wanafunzi
   D. Njia mbali mbali ya kuyatunza mazingira

<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali ya 6 - 10</u>



Binadamu wana mengi wanayoweza kujifunza kutoka kwa viumbe wenginewalioumbwa na Mungu. Viumbe ambao ni mfano bora kwa binadamu ni nyuki. Nyuki wanajulikana kwa mambo mawili makuu. Jambo la kwanza ni uwezo wao kuunda chakula kitamu kuliko vyote; asali. Jambo jingine ni ule uwezo wa wa kuwaangamiza watu au wanyama iwapo watamvamia kwa pamoja, Mawili hayo ni mambo wanayoweza kufanya licha ya kuwa na umbo dogo sana. Je, kwa nini mambo hayo huwezekana?

nyuki huwa na bidii sana. Utawaona wakiingia na kutoka katika mzinga wao tangu asubuhi hadi anya hivyo jua liwake au pawe na baridi. Wao si kama binadamu wengine ambao wanaweza